

Utakapofika Kilwa Kisiwani, utakutana na wenyiji waishio eneo hili la urithi. Kwa wenyiji hawa magofu muhimu zaidi ni misikiti na makaburi. Kwao ni sehemu takatifu za ibada na matambiko.

Wenyiji hutumia eneo la urithi kuelimisha wanafunzi hasa wa shule za msingi juu ya historia ya jamii yao pamoja na mahusiano yao na magofu.

Vilevile, wenyiji huwafurahisha wageni na ndugu zao kwa kuwatembeza katika magofu.



Kumbuka! Wakaazi wa Kilwa Kisiwani wanalithamini eneo la urithi kama nyumbani kwao. Utakapotembelea eneo hili, tafadhalii litumie kwa uangalifu.

- Utakapokutana na wenyiji wasalimie.
- Zingatia uvaaji wenyiji wasalimie. Usivae nguo zenyi kuacha wazi sehemu za mwili.
- Si sahihi kula hadharani wakati wa ramadhani, muongoza watalii atakuonyesha sehemu maalum ya kula.
- Eneo hili lina maziko ya watu. Usipande juu ya makaburi.
- Zingatia usafi wa eneo la urithi!

Mambo ya kuzingatia kabla ya kutembelea eneo la magofu

- Hakikisha unapata kibali kutoka ofisi ya Idara ya Mambo ya Kale iliyopo karibu na bandari
- Huduma ya chakula na vinywaji hupatikana Kisiwani wakati wote. Ongea na muongoza watalii kuweka oda ya chakula cha asili.
- Maliwato yanapatikana karibu na Kasri la Makutani na Husuni Kubwa.
- Kuwa huru kupiga picha magofu, lakini usipige watu picha bila ridhaa yao.
- Kuwa makini utembeapo, njia zingine siyo salama.



Asante



Arts & Humanities
Research Council



UNIVERSITY
of York

Shukurani

Idara ya Mambo ya Kale, Tanzania
Kilwa Islands Tours
Kamati ya Magofu na jamii ya Kilwa Kisiwani

Kilwa Kisiwani Eneo la Urithi wa Dunia

Karibu katika mji wa kale wa Waswahili na bandari maarufu zaidi katika Pwani ya Africa Mashariki. Mji huu ulishamiri kati ya karne ya 13 hadi 14 japo kua ulikaliwa tangu karne ya 9.



Kilwa Kisiwani ina magofu yanayovutia yaliyojengwa kwa kutumia matumbawe na chokaa kama vile

- Msikiti Mkuu ulioezekwa kwa paa la matungi yaliyorembwa kwa mabakuli ya Kiajemi.
- Husuni Kubwa, Kasri la karne ya 14 lenye bwawa la pekee kwaajili ya kuoga.
- Kasri la Makutani, makazi ya karne 18 yaliyozungukwa na ukuta mrefu. Kasri hili limejengwa na pesa za biashara ya watumwa.
- Ngome ya Wareno, ilikaliwa mwaka 1505 na wanaume 12 waliotawala biashara katika Kilwa. Ilifanyiwa upanuzi baadae na Waomani.
- Msikiti wa Malindi na makaburi nje ya msikiti huu yanahuishwa na familia kutoka Pwani ya Kenya.
- Nyumba za makazi, mfano nyumba iliyojengewa msikiti wake mdogo ndani.

Kilwa Kisiwani



Msikiti



Mwanzo ya njia




Njia za kupita



Maliwato



Gati



Kasri (Husuni Kubwa)

Unaweza kuona seti ya kuta katika umbo la pembe nane? Hilo ni bwawa! Ungejisikiaje kama ungeoaga katika bwawa hili kwa sasa?



Makaburi




Maziko na makaburi bado yana umuhimu mkubwa kwa wenyiji wa hapa, hivyo wanakuomba usiyakanyage. Kuwa mwangalifu unapopita!



Kijiji




Watu wa Kilwa Kisiwani wangependa kukutana na wewe. Tafadhalii watembelee kununua maji na kuwasalimu.




Msikiti mdogo

Angalia juu! Unaweza kuona mabakuli mazuri kwenye paa. Unapendelea lipi?




Msikiti Mkuu

Miguu yako imechoka? Imechafuka? Angalia pande kubwa la matumbawe karibu na mlango. Lilitumika kusafisha miguu kabla ya kuingia ndani.




Msikiti Mkuu

Chunga usianguke! Utakapofika Msikiti Mkuu, utakutana na mabaki ya viberenge yaliyotumiwa na watafiti wa kiakiolojia kusomba udongo.



Kasri la Makutani



Gereza (Fort)

Mawe yalikua ghali na magumu kuyasafirisha. Matumbawe ya aina mbalimbali yalichukuliwa kutoka baharini, na ilikua rahisi kuyatumia. Je, unaweza kuona matumbawe yenye umbo la feni, ubongo au mti?



Kutunza majengo ya miaka ya 1400 na kuonekana imara ni kazi kubwa sana. Kwasasa, watu huchukua matumbawe kutoka baharini, huyachoma kupata chokaa ambayo hulowekwa ili kuondoaa chumvi. Kisha huchanganywa na udongo pamoja na mchanga ili kuziba nyufa na kufanya kuta ziwe imara.